

# COVID-19: Kila mmoja ni muhimu

## *Aprili 2020*

Ushahidi uko wazi kwamba watu wenye umri mkubwa ni miongoni mwa wale walio katika hatari kubwa ya kupata madhara kutokana na COVID-19[1]. Kadri tunavyokuwa watu wazima maisha yetu hayapaswi kupoteza thamani. Wazee ni sisi, ni wanafamilia wetu, walezi wetu, wafanyakazi na majirani zetu.

Ugonjwa huu unatuathiri sote lakini utakuwa na athari kubwa kwa wale ambao wanakabiliwa na umaskini, afya duni na ubaguzi. Tunaweza tu kuzuia usambaaji wa virusi na kupunguza athari zake katika maisha yetu kama tutashirikiana katika jamii, taasisi na nchi mbalimbali.

Tunatoa wito kwa serikali, wahisani na mashirika kutambua hatari kubwa ambayo inawakabili wazee katika hadhi na ustawi wao katika ugonjwa huu, kusikiliza mawazo yao, kuhakikisha wanapata kwa usawa hatua za kujikinga, msaada na huduma katika mazingira yote. Serikali na mashirika yanatakiwa kuhakikisha kwamba sote tunajua hatua za kuchukua ili kujikinga sisi wenyewe, kukingana na kuwakinga walio hatarini zaidi. **Kila mmoja ni muhimu.**

**Mapendekezo**

1. Kufuata kanuni za usawa na kutokuwa na ubaguzi
2. Kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za afya na zilizo muhimu kwa wote
3. Kuhakikisha upatikanaji wa haki katika kinga na msaada kwenye maeneo yote
4. Kutoa fursa ya kupata ulinzi wa jamii na huduma kwa haki
5. Kutambua hatari kwa wazee katika maeneo yenye migogoro na ya wakimbizi na kutoa msaada bila kujali hadhi ya kisheria.
6. Kugawa fedha kwa uwazi kwa wale walio hatarini zaidi kwenye maeneo yote

7. Kuwa na mshikamano na jumuiya ya kimataifa
8. Kujenga mustakabali mzuri kwa ajili ya wazee

## 1. Kufuata kanuni za usawa na kutokuwa na ubaguzi

**Ushughulikiaji wa ugonjwa wa COVID-19 lazima ulingane na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu na kanuni zinazotumika kwa kila mmoja, kila mahali.**

Hii inamaanisha kwamba serikali lazima zifuate haki za wazee za kuwa na afya, ikiwa ni pamoja na kupata kwa misingi ya usawa huduma za afya, huduma za matibabu na taarifa kama watu wengine na bila ya ubaguzi. Kadri mahitaji yanavyoongezeka katika huduma za afya, kila mmoja lazima ahakikishiwe upatikanaji sawa wa matibabu ya kuokoa maisha anaouhitaji. Serikali na Shirika la Afya Duniani (WHO) wanapaswa kuweka taratibu za 'haraka' katika ugawaji wa rasilimali za matibabu zilizo chache. Taratibu hizo lazima zizingatie tathmini ya kimatibabu, mahitaji ya kitabibu, ushahidi wa kisayansi na kanuni za kimaadili, na sio katika sifa zisizo za kitabibu kama vile umri au ulemavu.

Hatua za dharura ambazo zinafanywa na serikali katika kupunguza au kuzuia usambaaji wa virusi lazima ziwe za muda mfupi, muhimu, zenye uwiano na zisiwe na ubaguzi unaozingatia umri au sifa nyingine yoyote kama vile jinsia au ulemavu. Sera za utengaji ambazo zinaweka masharti makali kwa wazee kwa kuzingatia umri wao ni za kibaguzi. Vikwazo katika haki nyingine, kama vile upatikanaji wa matunzo na huduma za msaada au hatua za ulinzi wa kijamii zitakuwa na athari za kutokuwa na uwiano kwa wazee ambao tayari wamesahauliwa au kutengwa, wenye mahitaji maalumu ya msaada, ambao hawama makazi au walemavu.

## 2. Kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za afya na zilizo muhimu kwa wote

**mawasiliano ya mara kwa mara na umma ni moja ya hatua muhimu sana za kuokoa maisha na kupunguza matokeo mabaya. Ni muhimu kwamba taarifa kuhusu COVID-19 inavyosambaa na kutibiwa, na tunachoweza kufanya ili kuzuia maambukizo kwetu wenyewe na kwa wengine, zipatikane na kuwafikia wahusika wote.**

*"Wazee walio wengi wanaogopeshwa na taarifa za vifo vingi kutoka katika nchi nyingine. Hii inasababisha hofu. Watu wenye miaka zaidi ya 80 hasa ndio wenye wasiwasi. Jambo muhimu sana ni kuwahakikishia watu, kitu ambacho ninajaribu kufanya. Ninawaambia: 'tumekutana na mengi sana katika maisha yetu; tutashinda katika hili pia"*

***Mwanamke mzee, Kyrgyzstan***

Taarifa za afya ya umma zinahitaji kutaja nani yuko katika hatari ya kupotea au kutengwa, ikiwa ni pamoja na wazee, ambao wanaweza kuwa na viwango vidogo vya elimu, wanaongea lugha za makabila tu au wana ulemavu. Pia wanaweza kuwa wanaishi maeneo ya mbali vijijini, maeneo yasiyo rasmi au makazi ya wakimbizi wa ndani ambako kunafanya iwe vigumu kuyafikia. Wazee wana haki ya kupata taarifa ili kufanya uchaguzi wakiwa na uelewa wa kutosha kuhusu afya zao wenyewe na kuwa na utulivu wa akili. Mara nyingi wazee wanaume na wanawake wana jukumu muhimu katika familia zao na za jirani na wanaweza kusaidia kusambaza taarifa, pamoja na kuchangia vizuri katika kutafuta suluhisho na kuchukua hatua ya kujikinga wenyewe na jamii zao.

Mamlaka za taifa na wengine lazima watoe mara kwa mara, taarifa za wazi na sahihi kuhusu hali halisi na uthibitisho wa hatua zao za ushughulikiaji. Hii inajumuisha data zilizochanganuliwa kwa umri, jinsi na ulemavu katika idadi ya wagonjwa na vifo. Tofauti za maambukizo na matokeo kati ya wazee wanawake na wanaume zichanganuliwe ili kueleza uandaaji wa hatua za kinga na ushughulikiaji wake.

Wakati ambapo wazee ni miongoni mwa wale walio katika hatari ya kupata madhara kutokana na COVID-19, huu sio 'ugonjwa wa mzee'. Taarifa zisizo sahihi zinachochea unyanyapaa na ubaguzi ambavyo wazee wengi tayari wanakabiliana navyo. Kila mmoja yuko katika hatari ya kuambukizwa COVID-19, na kila mmoja anaweza kusaidia kuzuia maambukizo.

## 3. Kuhakikisha upatikanaji wa usawa katika kinga na msaada kwenye maeneo yote

**serikali lazima zisaidiwe katika kutekeleza hatua kikamilifu kulingana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kupunguza maambukizo ya COVID-19 na kuhakikisha hakuna asiyefikiwa. Hatua mahususi ya kusaidia wazee katika maeneo yote lazima zitekelezwe na serikali  na mashirika ya misaada ya kibinadamu wakati wa mlipuko wa ugonjwa.**

*"Mara ya mwisho wazee walipolipwa ujira wao ilikuwa Januari walipopata malipo ya Novemba na Desemba. Kwa sasa, hawana fedha za kulipia pango ukiachia kumudu kununua akiba ya mahitaji muhimu kama uzuiaji wa mikusanyiko na kutembea utaongezwa."*

***Mwanamke mzee, Kenya***

Maoni na uzoefu wa wazee wenyewe unahitaji kusikilizwa katika mipango na utekelezaji wa ushughulikiaji wa COVID-19. Wazee wanaoishi peke yao au waliotengwa peke yao wanatakiwa kuwezeshwa kuwa na mawasiliano na familia na marafiki. Iwekwe mifumo ya kuhakikisha kwamba wazee wanaweza kuendelea kupata matunzo na msaada kama utahitajika, na mahitaji muhimu, ikiwa ni pamoja na chakula, maji safi na dawa. Wafanyakazi wa huduma na msaada wanatakiwa kuwa na vifaa vya kujilinda binafsi vinavyofaa na mwongozo wa wazi wa namna ya kujilinda wenyewe na wazee wanaowasaidia.

Kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka misongamano na kufunika pua na midomo yetu tunapokohoa au kupiga chafya, ni hatua muhimu za kupunguza maambukizo ya COVID-19. Hata hivyo, kunawa mikono na kuepuka misongamano ni rahisi kutekelezwa na baadhi kuliko wengine. Watu wengi, ikiwa ni pamoja na wazee, wanaishi bila ya kupata vifaa vya msingi vya kunawa mikono na usafi. Wazee wasio ma makazi wapatiwe nyumba mara moja. Wakati mwingine haiwezekani kuepuka misongamano kwa wale wanaoishi karibu, kama vile katika makazi yasiyo rasmi yenye idadi kubwa ya watu. Hii iwe muhimu kwa serikali kufuata ushauri wa Shirika la Afya Duniani wa kuwatenga, kuwapima, kuwatibu na kuwafuatilia wagonjwa wa COVID-19[2].

## 4. Kutoa fursa ya kupata ulinzi wa jamii na huduma kwa haki

**Kutokana na ugonjwa huu, vipato vya wazee na viwango vya maisha vinaweza kushuka sana na kuwaweka katika hatari kubwa ya matatizo ya kiuchumi. Serikali lazima ziendelee kulipa pensheni na kuongeza mifumo ya pensheni ili wazee wote wawe na kipato kizuri.**

*"Wanaotunza wazee kama mimi, lazima wapewe msaada maalumu. Mimi ni chanzo kikuu cha kipato kwa familia yangu na wananitegemea, lakini sasa sina kipato thabiti."*

***Mzee, Jordan***

Wazee wanaweza kutegemea vyanzo vingi vya kipato ikiwa ni pamoja na kazi za kulipwa, akiba, msaada wa fedha kutoka kwa familia na pensheni. Hata hivyo, baadhi ya vipato hivyo vinaweza kuwa vidogo na visivyo vya kawaida na wazee wengi hawapati pensheni. Wanawake wazee wana uwezekano mdogo wa kupata pensheni, mara nyingi wana akiba ndogo na wanamiliki mali chache.

Wanawake wa umri wote wanafanya kazi ya matunzo isiyowiana na malipo, ambayo inaweza kuwaweka katika hatari kubwa ya maambukizo. Mara nyingi wanawake wazee wanatunza wanafamilia na wanajamii, wakifanya kazi mara mbili  zaidi ya malipo ya wanaume wazee, hali ambayo inaweza kuongezeka katika dharura[3]. Ushughulikiaji unapaswa kuelekezwa katika uchanganuzi wa jinsia, kutathmini athari ya hatua zilizopendekezwa kwa wanawake wa umri wote na kuhakikisha wanapata kwa usawa kinga na msaada.

Wazee wote na hususan wazee wanawake wanakabiliwa na ongezeko la hatari ya ukatili majumbani - ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kimwili, kisaikolojia, kifedha na kingono - wakati wa utekelezaji wa hatua za kuepuka misongamano. Kuna ushahidi unaoonyesha kwamba ukatili wa majumbani umeongezeka tangu kuanza kwa mlipuko wa ugonjwa[4]. Katika kipindi cha ugonjwa huu na siku zijazo, wazee lazima waweze kuripoti matukio kwa usalama na kupata huduma. Serikali na watunga sera wanatakiwa kuhakikisha  huduma za kushughulikia ukatili na unyanyasaji zinapewa umuhimu na kujumuishwa katika mipango ya kujitayarisha na ushughulikiaji kwa ajili ya COVID-19, ikijumuisha mibadala ya kuwafanya wafikiwe wakati wa vipindi vya utengaji.

## 5. Kutambua hatari kwa wazee katika maeneo yenye migogoro na ya wakimbizi wa ndani na kutoa msaada bila ya kujali hadhi ya kisheria

**Hatari za muda mrefu kwa ustawi na hadhi ya wazee katika mazingira ya misaada ya kibinadamu lazima zitambuliwe na kushughulikiwa na mashirika ya misaada ya kibinadamu na serikali.**

*"Sijui chochote kuhusu virusi hivyo, ni watu tu wanasema kitu kuhusu virusi kwenye kipazasauti, lakini sisikii vizuri, ndio maana sijui chochote... wakati wote nafikiria, wanasema nini kwenye kipazasauti?"*

***Mwanamke mzee, Kambi ya wakimbizi ya Rohingya***

Credit: Amnesty International press release, 6 April 2020

Wazee walio katika maeneo yenye migogoro na ya wakimbizi wanakabiliwa na vikwazo vya muda mrefu vya kupata misaada ya kibinadamu, ambayo yanaongezeka katika kipindi cha COVID-19 na kuwaongezea hatari zaidi. Hii inajumuisha vikwazo vya kupata taarifa, huduma za afya na maji na miundombinu ya usafi, pamoja na ubaguzi wa umri katika ugawaji wa rasilimali adimu. Wanakabiliwa na hatari kubwa za madhara kutokana na maambukizo katika mazingira ambayo virusi vinaweza kusambaa haraka na ambapo vituo vya afya havina vifaa vya kutosha kuwashughulikia.

Serikali na mashirika ya kutoa misaada ya kibinadamu lazima yashughulikie hatari inayoongezeka kwa wazee, ikiwa ni pamoja na kuzungumza na wazee kuhusu hatua bora za kukidhi mahitaji yao. Wanahitaji kufanya jitihada za kuhakikisha maji na miundombinu ya usafi inapatikana kwa urahisi, na kwamba taarifa sahihi zinatolewa kwa wakati katika njia inayoweza kupatikana. Wazee wanaoishi katika maeneo ya wakimbizi lazima waweze kupata huduma za afya zinazotolewa na mfumo wa afya wa taifa, bila ya kujali hadhi ya kisheria.

Mpango wa Dunia wa Umoja wa Mataifa wa kushughulikia Misaada ya Kibinadamu[5] kwa ajili ya COVID-19 unapokewa lakini unashindwa kutambua na kutoa ipasavyo huduma inayofaa kwa changamoto nyingi zinazowakabili wazee. Wazee lazima wabainishwe miongoni mwa wale wanaoathirika zaidi na walio hatarini, na kulengwa kwa uwazi katika ushughulikiaji kama misaada ya kibinadamu ni kwa ajili ya kutekeleza wajibu wao na kuokoa maisha.

## 6. Kugawa fedha kwa uwazi kwa wale walio hatarini zaidi kwenye maeneo yote

**Wakati wote wazee wamekuwa hawaangaliwi katika maendeleo na uandaaji wa mkakati wa misaada ya kibinadamu na ugharimiaji. Ni wakati sasa wa jambo hili kubadilika.**

Hatari inayoletwa na COVID-19 katika hadhi na ustawi wa wazee inamaanisha wanahitaji kubainishwa kwa uwazi na kuzingatiwa katika maombi ya fedha na uamuzi katika ngazi zote na katika maeneo yote. Fedha lazima zipatikane kwa wadau wenye utaalamu sahihi, ikiwa ni pamoja na jamii za wenyeji na asasi ili kuhakikisha ushughulikiaji unakidhi mahitaji ya wale walio hatarini zaidi na walioathirika zaidi. Ugharimiaji ushughulikie mahitaji ya kiafya na athari za virusi kijamii na kiuchumi katika hatua zote mbili za ushughulikiaji na hatua ya kurejea katika hali ya kawaida.

## 7. Kuwa na mshikamano na jumuiya ya kimataifa

**Athari ya COVID-19 itakuwa kubwa kwenye nchi zenye uchumi wa chini na wa kati, ambako mifumo ya afya inaweza kuwa duni, hatua za kinga ni ngumu kutekeleza na wazee wanaweza kuwa hawana au wana ulinzi mdogo wa jamii. Nchi zenye uchumi mkubwa lazima zishirikishane rasilimali ili kuimarisha mifumo ya afya, kuongeza mipango ya ulinzi wa jamii na kusaidia ufufuaji wa uchumi wa nchi zenye kipato cha chini na cha kati.**

*"Awamu hii imenifanya nithamini mambo madogo, kinachonihusu hasa na wale wanaonijali. Pia imenikumbusha mambo ninayoyapenda, nilishona, nilisoma, nilitunza nyumba yangu kwa namna mbalimabli. Pia iliimarisha uhusiano wetu na wanafamilia na kufufua uhusiano wa zamani."*

***Mwanamke mzee, Lebanon***

Pia zinapaswa kushirikishana utendaji mzuri katika uzoefu wao wa kushughulikia ugonjwa huu na data za kuharakisha utafiti wa dunia wa kufanya ugunduzi, dawa na chanjo. COVID-19 haijali mipaka, hivyo nchi zinapaswa kushirikiana kupambana nayo. Tunahitaji ushughulikiaji wa nchi nyingi na uongozi thabiti kutoka katika vyombo vya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa na Shirika la Afya Duniani, ambao wanatambua kikamilifu na kushughulikia hatari kubwa inayowakabili wazee kutokana na COVID-19, hususan katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati. Nchi lazima ziwekeze rasilimali ili kuzuia maambukizo na kutoa matibabu bora kadri iwezekanavyo kwa wale wanaougua.

## 8. Kujenga mustakabali mzuri wa kuwajumuisha wazee

**Wengi wetu tutakumbana na mabadiliko ya maisha au kupata hasara isiyoelezeka wakati wa mlipuko. Lakini tutakuwa na nafasi ya kubadilisha dunia kuwa mahali bora.**

Uzoefu wetu wa COVID-19 unaonyesha umuhimu wa kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kujenga mifumo na jamii thabiti na imara kwa kila mmoja, wakiwemo na wazee.

Lazima tuwekeze katika mifumo ya afya ya umma kama sehemu ya kujenga usalama wa afya duniani na kuimarisha utoaji wa afya kwa kila mmoja ili kuhakikisha afya bora na ustawi wa watu wote kila mahali. Ni nafasi ya kuanzisha na kuimarisha mifumo ya ulinzi wa jamii, ikiwa ni pamoja na pensheni kwa wote, ambayo inahakikisha kipato cha kutosha kwa watu wote wanapokuwa wazee.

Ugonjwa huu umeonyesha jinsi ambavyo dunia yetu haiko sawa. Lazima tuhakikishe haki ya kila mmoja kuwa sawa na kutobaguliwa inatumika sasa na siku zijazo.

## Maandiko na miongozo zaidi

- HelpAge International COVID-19 hub
  www.helpage.org/coronavirus-covid19
- Advice on administering pensions, HelpAge International
  www.helpage.org/what-we-do/how-to-administer-pension-payments-during-the-covid19-pandemic
- Guidance on collecting pensions, HelpAge International
  www.helpage.org/what-we-do/how-older-people-can-safely-collect-pension-payments-during-the-covid19-pandemic
- Guidelines for care homes, HelpAge International
  www.helpage.org/what-we-do/guidelines-for-care-homes-for-older-people-in-the-context-of-coronavirus-covid19
- Advice for older people, HelpAge International
  www.helpage.org/download/5e809c5620653
- Advice for communities and older people's associations, HelpAge International
  www.helpage.org/what-we-do/covid19-guidance-and-advice-for-communities-and-older-peoples-associations
- Older people and COVID-19 in informal settlements, HelpAge International
  www.helpage.org/cities
- "Unacceptable" – UN expert urges better protection of older persons facing the highest risk of the COVID-19 pandemic, OHCHR

---

**HelpAge International ni mtandao wa kimataifa wa mashirika yanayohimiza haki kwa wazee wote kuishi maisha mazuri, yenye afya na usalama.**

Imechapishwa Aprili 2020 na HelpAge International, S.L.P 70156, London WC1A 9GB, Registered charity no. 288180

[1]Jordan R et al., 'COVID-19: risk factors for severe disease and death', The BMJ, 2020

Fai Zhou MD et al., 'Clinical course and risk factors for mortality of adult inpatients with COVID-19 in Wuhan, China: a retrospective cohort study', The Lancet, 2020

[2]World Economic Forum, *WHO coronavirus briefing: Isolation, testing and tracing comprise the 'backbone' of response*,https://www.weforum.org/agenda/2020/03/testing-tracing-backbone-who-coronavirus-wednesdays-briefing/ (15 Apr 2020)

[3]Overseas Development Institute, *Between work and care*, https://www.odi.org/sites/odi.org.uk/files/resource-documents/12509.pdf (15 Apr 2020)

[4]United Nations, *UN chief calls for domestic violence 'ceasefire' amid 'horrifying global surge'*,https://news.un.org/en/story/2020/04/1061052, (15 Apr 2020)

[5]United Nations, *Press Release COVID-19 Global Humanitarian Response Plan*,https://www.unicef.org/rosa/media/6171/file/PRESS%20RELEASE%20COVID-19%20Global%20Humanitarian%20Response%20Plan.pdf.pdf, (15 Apr 2020)